THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2:30 ***Jumatano, 12 Oktoba 2011 mchana***

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM

SEHEMU A: QUR'AN

1. Bainisha hatua sita alizochukua Mtume (s.a.w) katika kuhifadhi Qur'an katika msahafu.

2. Andika tafsiri ya suratul-Tyn (95:1-8) na kisha toa mafunzo matano yatokanayo na sura hii.

3. Jadili vipengele vinne kuonesha udhaifu wa makafiri wenye fikra kuwa Qur'an ni aya za shetani.

SEHEMU B: TAWHIID

4. Kumuamini Mwenyezi Mungu si suala la kibubusa (kufuata mkumbo) bali ni suala la kitaaluma. Kwa kurejea Qur'an toa hoja sita kuthibitisha kauli hii.

5. Thibitisha kwa hoja sita kuwa kuwepo maisha ya akhera ni jambo lisiloepukika.

6. Nguzo ya tatu ya imani ni kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu. Lakini katika vitabu vyote vilivyofunuliwa, Qur'an inatofautiana na vitabu vingine vyote. Jadili tofauti nne zilizopo kati ya Qur 'an na vitabu hivyo.

SEHEMU C: FIQH

7. Onesha katika vipengele vinne namna utakavyoikafini maiti ya Muislamu mwanaume.

8. Jadili kwa kina vipengele sita kuhusu wajibu wa wazazi juu ya malezi bora ya watoto.

9. Lengo la swala kama lilivyotajwa kwenye Qur-an ni kumzuia mwenye kuswali na mambo machafu na maovu kama inavyooneshwa katika sura Al-Ankabuut. *" Bila shaka sala (ikisaliwa vilivyo) humzuilia (huyo mwenye kusali na) mambo machafu na maovu..." (29 :45).*
Eleza vipengele vinne vinavyoonesha namna swala inavyomtakasa mja kimwili na kiroho (kiutu).

Scanned by CamScanner

SEHEMU D: TAREKH

10. Kwa kutumia hoja sita, thibitisha kauli hii: "Umar bin Abdul-Aziz ni Khalifa wa tano wa Mtume (s.a.w)."

11. Eleza sababu sita zilizopelekea "riddah" hadi kuuliwa khalifa Uthman.

12. Chambua mafunzo sita kwa Waislamu wa leo kutokana na Hijra ya Mtume (s.a.w) kwenda Madina.

Scanned by CamScanner